

UFUNDI MAAGIZO

Mashujaa wa Imani, Kitengo cha 3



NYANGUMI


VIFAA

- Kiolezo
- Kalamu ya alama/kalamu
- Mkasi
- Rangi
-



MAAGIZO

1. Kata vipande vya muundo wa nyangumi na uvipake rangi.
2. Gundisha mkia wa kipande cha 1 juu ya mkia wa kipande cha 2. Vinapokauka, vikunje kuelekea juu katika vistari katika mwisho wa kipande cha 2. Gundisha mwisho wa kipande cha 1 kwenye sehemu iliyokunjwa ya kipande cha 2 ili nyangumi jiwe na sehemu ya juu ilikunjwa.
3. Kipande cha 3 ni mdomo. Chora mfupanyangumi (meno) na ugundishe mbele ya nyangumi. Gundisha macho juu ya mdomo na uchore nukta kwa ajili ya mboni ya jicho.
4. Kwenye kipande cha 5, kata mistari yote kwenye upande mmoja. Unapomaliza, kunja karatasi na ugundishe juu ya nyangumi kama maji yanayorushwa kutoka kwa tundu la pua.
5. Ili kumaliza ufundi, chora mistari kadhaa kwenye pezi ya mkia.



NAAMANI KWENYE MTO

VIFAA

- Karatasi ya povu ya bluu au ya rangi
- Vijiti vya mbao vya popsika
- Picha ya Naamani akiwa na ukoma na bila ukoma
- Rangi
- Mkasi
- Gundi



MAAGIZO

1. Kata vipande: mawimbi 3 kwa kila mtoto na karatasi 2 za Naamani, moja akiwa na ukoma na nyingine bila ukoma.
2. Ikiwa mawimbi ni meupe, yapake rangi yafanane na maji. Gundisha mawimbi pamoja. Weka gundi tu katika upande wa juu ya mawimbi katika karatasi moja na ugundishe katika kingo ya wimbi lingine hadi uwe umeunganisha mawimbi matatu. Ruhusa yakauke.
3. Baada ya kukauka, gundisha pande zote mbili pamoja ili kuunda tyubu.

4. Paka rangi kwenye vipande vyote vya Naamani. Weka Naamani mmoja akiwa ameangalia upande wa chini na ugundishe kijiti. .Kisha chukua kipande kingine cha Naamani na ugundishe juu ya kijiti ili oanishe na kipande cha kwanza.
5. Ili kucheza na ufundi, shika kijiti ndani ya tyubu ya mpepeo wakati Naamani akiwa juu ya maji. Kwanza, anaanza na ukoma, kisha baada ya kuzama mara 7 ndani ya maji, anakuwa msafi!

ALAMISHO YA SIMBA

VIFAA

- Karatasi ya mduara kama umekata kulingana na mistari
- Macho 2 madogo ya yanayosonga
- Kijiko cha plastiki au kijiti cha popsika
- Kalamu ya alama/kalamu
- Gundi
- Rangi



MAAGIZO

1. Paka rangi mduara na utoboe mstari ndani ya mduara kwa ajili ya kijiko au kijiti. Kata mistari kuzunguka kingo ili kuunda pindo. Kuwa mwangalifu usikate hadi kufikia mstari ndani ya mduara.
2. Ingiza kijiko au kijiti kupitia sehemu iliyotobolewa na ugundishe.
3. Gundisha macho na kwa kutumia kalamu ya alama chora pua na mdomo. Unaweza kuchora macho badala ya kutumia macho yanayosonga.
4. Alamisho yako iko tayari!